


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO



SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA
(COASCO)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CA.61/287/01/32

Tarehe: 28.05.2026

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,

Vyama vya Ushirika,

TANZANIA BARA

Yah: **MWALIKO WA MAFUNZO YA KITAALAM KWA BODI NA WATENDAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUHUSU MASUALA YA UONGOZI, KODI, UHASIBU NA TEHAMA**

Husika na Kichwa cha Habari hapo juu.

2. Moja ya jukumu la COASCO kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu Na 4 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika Sura ya 185 toleo la Mwaka 2023 ni kutoa Ushauri na mafunzo kwa Vyama vya Ushirika na wateja wengine ili kuwajengea uwezo wa utendaji, usimamizi wa rasilimali na uandaaji wa taarifa za fedha unaozingatia viwango vya uhasibu vya kimataifa.

3. Hivyo, **COASCO** imeandaa mafunzo maalum kwa nadharia na vitendo kwa muda wa siku tatu juu ya masuala ya uongozi, kodi, uhasibu na TEHAMA kwa **Bodi na Watendaji** (mada husika zimeambatanishwa). Mafunzo hayo yatafanyika katika ukumbi wa Destiny Kibaha tarehe 17 hadi 19 Juni, 2026 kuanzia saa mbili kamili asubuhi.


3. Gharama za mafunzo kwa kila mshiriki ni Tshs 350,000 ambayo inajumuisha mafunzo ya siku tatu, ukumbi, chai na chakula cha mchana. **Malipo hayo yatalipwa kupitia nambari ya malipo ya Serikali** itakayotolewa baada ya kuthibitisha ushiriki wako kwa kuwasiliana na RCA au mratibu wa mfunzo (CPA Anna Thomas) kupitia **nambari ya simu**

0658 732 050 au barua pepe anna.shao@coasco.go.tz

4. Ili kuwezesha maandalizi ya mafunzo haya unaombwa kuthibitisha ushiriki wako kwa wakati na malipo yafanyike mnamo au kabla ya **Tarehe 12.06.2026**.

Natanguliza shukrani.

Pamoja tujenge Uchumi



CPA Anna Thomas

KNY: MKURUGENZI MKUU

Nakala - Mrajis wa Vyama vya Ushirika – Dodoma

- Warajis wasaidizi wa Vyama vya Ushirika – **Tanzania Bara,**
- Wakaguzi wa Ushirika wa Mikoa (RCA) – **COASCO Tanzania Bara,**
- Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) – **Dar Es Salaam**
- Chama Kikuu Cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT) –
Dar Es Salaam

MADA ZITAKAZOFUNDISHWA

1. Mafunzo ya Kodi na Sheria za Kodi

Mada zitakazofundishwa ni pamoja na:

- Mipango ya kimkakati ya kodi na uzingatiaji wa sheria za kodi
- Jukumu la wahasibu na wakaguzi wa ndani katika ukaguzi wa kodi
- Ujazaji wa ritani za mwisho wa mwaka

2. Mafunzo ya TEHAMA na Advanced Excel

Mafunzo haya yatawajengea washiriki uwezo wa kutumia Excel kwa kiwango cha juu katika shughuli za kifedha. Mada zitahusisha:

- Uhamasishaji wa usalama wa mtandao na mbinu bora
- Uhamasishaji wa faragha ya data na uzingatiaji wa kanuni
- Usimamizi wa makubaliano ya kiwango cha huduma (SLA)
- Ununuzi wa mifumo na uendelezaji wa mifumo
- Vitendaji vya IF na LOOKUP – Fomula za Kimantiki kwa Maamuzi ya Uhasibu
- INDEX MATCH na XLOOKUP – Upatikanaji wa Data wa Hali ya Juu na Marejeleo ya Kibinafsi

3. Mafunzo ya Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka (IFRS)

Mafunzo haya yatazingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu (IFRS) katika uandaaji wa taarifa za fedha. Mada zitajumuisha:

- Uchambuzi wa viwango vya kifedha (ratio analysis)
- IAS 21: Athari za Mabadiliko ya Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni
- TFRS 1: Taarifa ya wenye mamlaka

4. Uongozi na maendeleo (Leadership & organization development)

Mafunzo haya yatalenga kuwawezesha washiriki kuelewa maswala ya uongozi. Mada ni pamoja na:

- Kuimarisha Utamaduni wa Taasisi kupitia uongozi madhubuti
- Ukuzaji, ugawaji madaraka na ushirikiano katika kutekeleza majukumu
- Usimamizi wa muda na tija

5. Hesabu ya mazao (Crop realization account)

Mafunzo haya yatalenga kuwawezesha washiriki kuelewa hesabu ya mazao. Mada ni pamoja na:

- Hesabu ya zao la Tumbaku
- Hesabu ya zao la Kahawa
- Hesabu ya zao la Korosho
- Hesabu ya mazao kwa ujumla

6. Usimamizi wa biashara ya usafirishaji

Mafunzo haya yatalenga kuwawezesha washiriki kuelewa biashara ya usafirishaji faida, udhibiti, na changamoto zake. Mada ni pamoja na:

- Msingi wa biashara ya usafirishaji
- Udhibiti wa fedha
- Usimamizi wa magari na uendeshaji
- Huduma kwa wateja na masoko
- Hatari usalama na sheria
- Teknolojia na maendeleo